ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

*Supplement No. 40* *24th October, 2025*

*SUBSIDIARY LEGISLATION*

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 37 Vol. 106 Dated 24thOctober, 2025*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI Na. 617 la tarehe 24/10/2025

SHERIA YA SIKUKUU ZA KITAIFA,
(SURA YA 35)

# TAMKO

***(Limetolewa chini ya kifungu cha 3)***

**TAMKO LA KUTANGAZA SIKU YA UCHAGUZI MKUU KUWA SIKU YA MAPUMZIKO, 2025**

**KWA KUWA** kifungu cha 3 cha Sheria ya Sikukuu za Kitaifa, Sura ya 35 kinampa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka ya kuteua siku yoyote tofauti na siku zilizoorodheshwa kwenye Jedwali ya Sheria hiyo na kuitamka siku hiyo kuwa siku ya mapumziko.

**NA KWA KUWA** kwa madhumuni ya kuwawezesha wananchi wote wenye sifa kutumia haki yao ya kikatiba kupiga kura, Rais ameona ni muhimu kutangaza Siku ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kuwa siku ya mapumziko;

**NA KWA KUWA** Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imetangaza kuwa Jumatano ya tarehe **29 Oktoba, 2025**, ambayo ni siku ya kazi, kuwa ndiyo siku ya uchaguzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025**;**

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

**HIVYO BASI,** kwa kutumia mamlaka niliyopewa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Sikukuu za Kitaifa, Sura ya 35, Mimi**, SAMIA SULUHU HASSAN,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninatangaza rasmi kuwa tarehe **29 Oktoba, 2025** itakuwa siku ya mapumziko**.**

Hati hii imethibitishwa kwa saini yangu na kuwekwa Lakiri ya Umma leo tarehe 22 Oktoba, 2025.

**L.S**

**Ikulu**
**Dodoma**

**SAMIA SULUHU HASSAN**
***Rais***

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA